

## HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO

Simu Na. 0737 205318  
Nukushi: 0732 951 745  
Barua pepe: [ded.busokelo@mbeya.go.tz](mailto:ded.busokelo@mbeya.go.tz)



Mkurugenzi Mtendaji,  
S. L. P. 2,  
**TUKUYU.**

Kumb. Na. BDC/J:2/02/Vol.V/90

06 Aprili, 2018.

### TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

1. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo anapenda kuwatangazia wananchi wote wa Tanzania wenye sifa za kuajiriwa katika Utumishi wa Umma kuomba kazi kwa nafasi ya **MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III** kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

#### 1.0 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (NAFASI 7)

##### (A) SIFA ZA MWOMBAJI:

- I. Awe na cheti cha kuhitimu na kufaulu kidato cha Nne (IV)
  - au cha Sita (VI);
- II. Aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika fani ya Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali;
- III. Awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwadilifu, mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 45;
- IV. Mwenye tabia njema isiyotia shaka na ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la Jinai;
- V. Awe tayari kufanya kazi katika Kijiji chochote kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

##### (B) KAZI/MAJUKUMU:

- I. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji;
- II. Kuwa mlinzi wa Amani na Usimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji;
- III. Kuratibu na Kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji;
- IV. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji;

- V. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu;
- VI. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ili kuondoa umaskini na kuongeza uzalishaji mali;
- VII. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji;
- VIII. Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo kwenye Kijiji;
- IX. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji;
- X. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wnanchi;

**(C) MSHAHARA:**

Atalipwa mshahara katika ngazi ya TGS B.

**1.1 JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Barua zote ziandikwe kwa mkono wa mwombaji na kutumwa kwa anwani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO,  
S. L. P 2,  
TUKUYU.**

**1.2 MUHIMU:**

- (a) Barua zinaweza kutumwa kwa njia ya Posta kwa walio mbali na walio jirani, wanaweza kuleta kwa njia mkono;
- (b) Barua/Anwani unayotumia kwa sasa pamoja na namba za simu viambatanishwe na:
- Maelezo Binafsi (CV),
  - Nakala ya vyeti vya taaluma,
  - Nakala ya cheti cha kuzaliwa,
  - Picha 2 za Passport Size za hivi karibuni.
- (c) Awe hajawahi patikana na kosa lolote la jinai;
- (d) Testimonials na Provisional Results havitakubalika;
- (e) Nakala zote za vyeti zithibitishwe na Hakimu au Wakili yeyote aliyesajiliwa na kuthibitishwa;

- (f) Watakaochaguliwa kuhudhuria usaili (Short-listed) watafahamishwa kupitia anwani na namba za simu walizoandika kwenye barua zao za maombi ya kazi.

**NB: Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 20 Aprili, 2018 siku ya Ijumaa saa 9:30 Alasiri.**

Aidha, tangazo hili waweza kulipata kupitia Tovuti ya [www.busokelodc.go.tz](http://www.busokelodc.go.tz)

Limetolewa na;



Eston Paul Ngilangwa  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO**

**DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR**  
**BUSOKELO DISTRICT COUNCIL**

**Nakala:**

1. Mbao zote za matangazo, Halmashauri, Ofisi za Kata na Vijiji.